

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anwani ya simu: “REGCOM COAST”  
Simu Na. 02-2402500.  
Fax Na. 02-2402250/2402686/2402151  
Barua pepe: [ras@pwani.go.tz](mailto:ras@pwani.go.tz)  
[ras.pwani@tamisemi.go.tz](mailto:ras.pwani@tamisemi.go.tz)



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
Mkoa wa Pwani,  
S. L. P 30080,  
**KIBAHA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**AWAMU YA KWANZA YA VIWANDA VILIVYOWEKEWA MAWE YA  
MSINGI NA MHESHIMIWA ENG. EVARIST NDIKILO MKUU WA  
MKOA WA PWANI TAREHE 14 AGOSTI HADI 27 AGOSTI 2019.**

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Pwani amehitimisha ziara yake ya awamu ya kwanza ya uwekaji wa mawe ya Msingi kwenye Viwanda katika Wilaya za ***Bagamoyo, Kibaha, Mkuranga na Rufiji.***

Katika awamu hiyo amepata fursa ya kuweka mawe ya Msingi kwenye viwanda kumi na tatu (13), amefungua Kiwanda kimoja (1) na kukagua shughuli za ujenzi za kiwanda kimoja (1).

Viwanda hivi vyote vitagharimu zaidi ya shilingi Bilioni 154.1 na vitatengeneza ajira zaidi ya 2,091 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 5000.

Viwanda alivyoweka mawe ya Msingi ni hivi vifuatavyo:-

<b>Na</b>	<b>Jina la Kiwanda</b>	<b>Bidhaa inayozalishwa/ itakayozaliswa</b>	<b>Mahali kilipo</b>	<b>Mtaji uliowekezwa</b>
1	H&J Fibre Investment Co. Ltd	Nyuzi	Pingo	Bilioni 33
2	Lake Steel and Allied Product Ltd	Nondo	Misugusugu	Bilioni 8.8
3	Lake Gas Cylinder Ltd	Mitungi ya Gesi	Misugusugu	Bilioni 15.4
4	Gravita Tanzania Ltd	Risasi na Aluminium	Zegereni	Bilioni 4.4
5	Roya I Super Market (2008) Ltd	Mikate	Zegereni	Bilioni 10
6	China Boda Technical Group Co. Ltd	Risasi ( Lead)	TAMCO Kibaha	Bilioni 26
7	Tanzania Huafeng Agriculture Development Ltd	Kuchakata Muhogo	Mkenge Mkuranga	Bilioni 9.1
8	Super Meals Limited	Maji (Cool Blue)	Viazi Mkuranga	Bilioni 2
9	Shafa Tanzania Investment	Matofali	Kisemvule Mkuranga	Bilioni 15.3
10	Maxima Industries (T) Ltd	Masufuria	Mkuranga	Bilioni 2
11	Textrade Limited	Kamba za Uvuvi	Kisemvule Mkuranga	Milioni 650
12	Plug In Limited	Nyaya za umeme	Kisemvule Mkuranga	Milioni 650
13	Huatang Investment Group Co. Ltd	Kuchakata Betri	Nyamwage Rufiji	Bilioni 13.2
14	Mothers Dairy Ltd	Kusindika Maziwa	Ikwiriri Rufiji	Milioni 300
15	Hester Bioscience Africa Limited	Kuzalisha Chanjo za Mifugo <b>(Ametembelea)</b>	TAMCO Kibaha	Bilioni 39.6

Ziara hiyo ililenga pia kutatua changamoto wanazokumbana nazo wawekezaji katika hatua za uwekezaji walizopo na kuhamasisha wawekezaji wengi kuja kuwekeza katika Mkoa wa Pwani. Aidha ziara hii imekuwa kielelezo tosha kwamba Tanzania hususani Mkoa wa Pwani uwekezaji unafanyika na wawekezaji wengi wanamuunga mkono Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka Nchi yetu katika Uchumi wa Kati unaotegemea viwanda.

Imetolewa na;

**OFISI YA MKUU WA MKOA WA PWANI.**

**28/08/2019**